

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA




Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini

KUINGIA KWENYE MABASI YA MIJINI KWA FUJO

FUJO

USTAARABU

1985 → 2021



2022 →

MPANGO WA KUHAMASISHA ABIRIA KUPANDA MABASI YA MIJINI KWA KUFUATA MSTARI

1.0 Utangulizi.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 31(1) (d) cha Sheria ya LATRA, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa huduma za Usafiri Ardhini, linajukumu la kushauriana na wadau, Serikali na makundi ya watumiaji huduma zinazodhibitiwa. Kwa mwaka wa Fedha 2021/22 Baraza linakusudia kuondoa changamoto, ya abiria kuingia kwenye vyombo vyaa usafiri kwa fujo (kupigania kuingia ndani ya basi).

Kwa muda mrefu sana abiria wa mabasi ya Mijini, wamekuwa wakiingia kwenye mabasi, kwa fujo bila kufuata utaratibu wa kistaarabu. Wengine huingilia pia kwa kupitia madirishani. Hali hii, huwafanya watoto, wazee, akina mama wajawazito, wagonjwa kuchelewa sana kupaata huduma ya usafiri hatakama wamewahi kufika kwenye vituo vyaa mabasi (daladala/mwendo kasi). Aidha, hali hii pia imeathiri saikolojia zawatumiaji wa usafiri wa Mijini. Wenye uwezo wa fedha, hununua magari binafsi, jambo ambalo huchangia kwa kiwango kikubwa kuongeza misongamano ya magari mijini.

Baraza, linakusudia kuhamasisha Jamii yote ya Tanzania kurudia ustaarabu wa miaka ya 1970 hadi 1984 wa kupanda mabasi kwa mistari.

Malengo ya Azma hii ni pamoja na:

1. Abiria wa kwanza kufika kwenye kituo, kuwa wakwanza kupata huduma ya usafiri kiustaarabu;
2. Kuwawezesha watoto, wazee, akina mama wajawazito, wagonjwa na abiria wote kupata huduma stahiki, kwa wakati;
3. Kujenga jamii iliyostaarabika;
4. Kuponya majeraha ya muda mrefu ya abiria kuteseka vituoni
5. Kutunza vyombo vyaa usafiri (Milango na madirisha)

6. Kuepusha ajali na majeraha ya mwili, kupunguza uwezekano wa maambukizi ya magonjwa
7. Kuongeza, utu, umoja, upendo, mshikamano katika jamii

2.0 Abiria kupanda mabasi kistaarabu;

Ili kufikia azma ya abiria kupanda mabasi kistaarabu (kwa mstari) yafuatayo yanahitajika:

(a) Mikutano ya hadhara ya wadau, kupata maoni mbalimbali.

(b) Viongozi wa Mbalimbali kushirikishwa

(c) Kutoa hamasa kwa jamii kwa kuititia:

- TV
- Radio/mitandao ya Kijamii

(d) **Uzinduzi rasmi, ufanyike kwa msisitizo Mikoa Mikubwa kama Dar es salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Arusha**

3.0 Hitimisho

Abiria kuweza kupanda mabasi kwa ustaarabu, kutaboresha huduma za usafiri nchini, kupunguza gharama za usafiri, foleni za magari barabarani na kuimarisha pato la Taifa. Hima tuungane sote kuhimiza abiria wote kupanda na kushuka kwenye mabasi kistaarabu.

KUBADILISHA TABIA YA ABIRIA KUINGIA KWENYE MABASI KWA FUJO.

TAREHE 01 Julai – 31 Dicemba, 2022

Tatizo/ker o	Chanzo	Madhara	Njia ya Utatuza	Wadau	Hatua za Utekelez
Abiria kuingia kwenye mabasi kwa fujo	<ul style="list-style-type: none"> • Kukosa ustaarabu • Tabia ya madereva • Usimamizi hafifu • Uchache wa mabasi 	<ul style="list-style-type: none"> • Jamii kuathirika Kisaikolojia (Hasa watoto, wazee, wajawazito) • Mwili kuumizwa (Ajali) 	<p>Abiria kuhamasishwa kukaa kwenye folen (mstari) wakati afikapo kwenye kituo chochote cha basi.</p>	Wadau Kiongozi Wadau Muhimu <ul style="list-style-type: none"> • LATRA • LATRA CCC • POLIS – U/Bara barani 	Angalia Mpango 1.

		<ul style="list-style-type: none"> • Kugombana kwenye vyombo vyatofauti • Chuki, hasira • Kuibiwa • Maambukizi ya magonjwa • Udhaliishaji • Kuchafuka 		<ul style="list-style-type: none"> • TANRO ADS • Asasi za Kijamii • Mashiri ka ya Kimata ifa • Halmas hari Mbalim bali • Wamili ki wa Vyomb o • Madere va wote • Abiria Wote
--	--	---	--	---